ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

*Supplement No. 39* *30th September, 2022*

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 40 Vol. 103 Dated 30th September, 2022*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 589 la tarehe 30/9/2022

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA YA 290

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya Vifungu vya 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MAZAO) ZA HALMASHAURI YA WILAYA NSIMBO ZA MWAKA 2022

Jina 1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo za Mwaka 2022.

Tafsiri 3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa au kufafanuliwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake afisa yeyote atakayeteuliwa na Mkurugenzi kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo na ni pamoja na Afisa yeyote wa Halmashauri atakayekuwa anatekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Kituo cha Ununuzi wa Mazao" maana yake ni eneo lilioainishwa na kutangazwa na Halmashauri kama kituo cha ununuzi wa mazao

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoingia mkataba na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri,

Utozaji wa ushuru na ada

4. (1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa kila biashara ya mazao inayofanyika katika eneo lililoainishwa na Halmashauri kama kituo cha ununuzi wa mazao.

(2) Ushuru wa mazao utatozwa na Halmashauri kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi na utatozwa kwa mnunuzi.

Namna ya kukusanya Ushuru katika kituo

5. (1) Bila kuathiri masharti ya Kifungu cha 4 cha Sheria Ndogo hizi, Halmashauri itaweka utaratibu wa kukusanya ushuru wa mazao katika kituo cha ununuzi kwa kadiri itakavyoona inafaa ikiwa ni pamoja na kutenga au kuainisha vituo maalumu vitakavyotumika kama vituo vya ununuzi wa mazao.

(2) Malipo ya ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala na kutolewa stakabadhi halali ya kielektroniki kama uthibitisho wa malipo yaliyofanyika.

(3) Halmashauri au Wakala atakuwa na mamlaka ya kukamata bidhaa au mali ya mtu yeyote endapo mtu huyo ameshindwa kulipa ushuru ndani ya muda aliotakiwa kulipa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(4) Endapo mali au bidhaa iliyokamatwa na Halmashauri au Wakala haitalipiwa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa zilizokamatwa na kiasi cha fedha kitakachopatikana baada ya bidhaa hizo kuuzwa kitarejeshwa kwa aliyekuwa mmiliki wa mali au

bidhaa hizo baada ya kutoa ushuru unaodaiwa, gharama za Mahakama, ukamataji, utunzaji na mnada na faini.

(5) Wakala hataruhusiwa kuuza au kufanya jambo lolote kwa mali au bidhaa iliyokamatwa bila kupata idhini ya Halmashauri.

Wajibu wa kulipa ushuru katika kituo

6. Kila mfanyabiashara au mnunuzi katika eneo la kituo cha ununuzi wa mazao atakuwa na wajibu wa:-

(a) kulipa kiwango cha ushuru kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi;
(b) kutoa taarifa sahihi kwa Halmashauri, Msimamizi wa kituo au Wakala kuhusu bidhaa zinazotakiwa kulipiwa ushuru;
(c) kutunza kumbukumbu za malipo;
(d) kutumia mzani uliohakikiwa na kuthibishwa na Wakala wa Vipimo Tanzania;
(e) Kuomba na kulipia vibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(f) kuwa na Leseni halali ya biashara iliyotolewa na Halmashauri;
(g) kununua mazao katika kituo kilichoainishwa na Halmashauri; na
(h) kuzingatia na kutimiza masharti ya kibali atakachokuwa amepewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Muda wa biashara

7. (1) Kila kituo cha ununuzi wa mazao kitafunguliwa kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa moja kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), ununuzi wa mazao utafanyika katika maeneo ambayo yatapangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

Halmashauri kuidhinisha Vituo

8. Halmashauri itaainisha vituo vitakavyotumika kwa ajili ya ununuzi wa mazao kabla ya kuanza kwa kila msimu wa kilimo na kuvitambulisha kwa Umma.

Sifa za kituo cha Ununuzi wa Mazao

9. Kituo cha ununuzi wa mazao kitatakiwa kuwa na:

(a) barabara ya kuwezesha magari ya mizigo kuingia na kutoka kwa urahisi;
(b) ukaribu na maeneo ya uzalishaji ambapo wakulima wanaweza kufikisha mazao na

kuuza kwa urahisi;

(c) huduma za kijamii kama vyoo;

(d) eneo la wakulima wanaoingiza bidhaa na eneo la wanunuzi wanao nunua na kutoa bidhaa;

(e) ulinzi wa mara kwa mara hasa kipindi ambacho biashara za mazao zinapofanyika; na

(f) vifaa vya kuhakiki na kupima ubora wa mazao wakati wa ununuzi.

Kibali cha Ununuzi wa Mazao

10. (1) Mtu au Kampuni yoyote kabla ya kuanza kununua mazao katika kituo cha ununuzi wa mazao atatakiwa kujisajili rasmi kama mnunuzi wa mazao na kuomba kibali cha ununuzi wa mazao kutoka Halmashauri

(2) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitakuwa katika fomu maalumu na kitaeleza aina ya mazao yatakayonunuliwa na kituo au vituo yatakaponunuliwa. Kibali kinachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitalipiwa ada ya shilingi Elfu Kumi tu (10,000/=) kwa mwaka

(3) Kibali kitatolewa kwa Mnunuzi mwenye Leseni halali ya Biashara iliyotolewa na Halmashauri

(4) Mnunuzi wa mazao atatakiwa kuzingatia masharti ya kibali chake.

Vibali vingine

11. (1) Mkulima atakayekuwa anataka kusafirisha mazao yake kutoka shambani kwenda stoo au kwenye ghala kwa ajili ya kuhifadhi atatakiwa kuomba kibali kwa Mtendaji wa Kijiji na baada ya idhini kutolewa na Mkurugenzi ataruhusiwa kusafirisha

(2) Kibali kitakachotolewa chini ya kifungu kidogo kitatolewa bure na Halmashauri itatakiwa kuhakikisha ofisi zote za Watendaji wa vijiji zinakuwa na vibali.

(3) Mtu yeyote atakayekuwa anasafirisha mazao kutoka eneo la Halmashauri atatakiwa kuomba kibali cha kusafirisha mazao nje ya eneo la Halmashauri

(4) Maombi ya kibali chini ya kifungu kidogo cha tatu yatatakiwa kuambatishwa na nyaraka zifuatazo;-

i) Stakabadhi halali ya malipo ya ushuru,

ii) Leseni halali ya biashara iliyotolewa na Halmashauri,

iii) Kibali cha ununuzi wa Mazao.

Uteuzi wa Msimamizi wa Kituo

12. Mkurugenzi atateua msimamizi kwa kila kituo cha ununuzi wa mazao ambao watakuwa na majukumu ya;-

(a) Kuorodhesha wakulima kwenye fomu maalumu itakayoonesha jina la kituo, jina la mkulima, aina ya zao, kiasi alichouza kwa kilo, namba ya simu ya mkulima

(b) Kuhakikisha wanunuzi wenye sifa ndio wananunua mazao katika kituo

(c) Kuhakikisha wanunuzi wananunua mazao kwa kutumia mzani uliohakikiwa na kuthibitishwa na Wakala wa Vipimo Tanzania

(d) Kuhakikisha anatunza kumbukumbu zote za ununuzi wa mazao katika kituo

(e) Kutoa taarifa za ununuzi wa mazao kwa Mtendaji wa Kata ambaye atatakiwa kuziwasilisha kwa Mkurugenzi kwa kadiri atakavyoelekezwa.

(f) Kuhakikisha wanunuzi wanaweka mazao kwenye vifungashio kwa kuzingatia ujazo unaotambulika kisheria

(g) Kuhakikisha mazao yote yanayotolewa na wanunuzi yamelipiwa ushuru wa Halmashauri.

(h) Kuhakikisha huduma muhimu kama choo zinapatikana.

(i) Kuhakikisha Kituo kinakuwa katika hali ya usafi na usalama wakati wote wa ununuzi wa mazao.

(j) Kusimamiana kuratibu shughuli zote katika kituo.

Rejista katika kituo cha ununuzi wa mazao

13. Kutakuwa na Rejista kwenye kila kituo cha ununuzi wa mazao ambapo kila mkulima na mnunuzi watatakiwa kujaza taarifa zao.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

14. (1) Halmashauri au Wakala wake anaweza kukamata na kuzuia chombo chochote cha usafiri kilichobeba mazao ya mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipia kibali au ushuru au hajanunua mazao katika kituo kilichoainishwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria Ndogo hizi.

(2) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa zilizokamatwa na kiasi cha fedha kitakachopatikana baada ya bidhaa hizo kuuzwa kitarejeshwa kwa aliyekuwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ushuru unaodaiwa, gharama za Mahakama, ukamataji, utunzaji na mnada na faini.

(3) Wakala hataruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(4) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo umesababishwa na Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa wakala

15. (1) Halmashauri inaweza kuteua wakala kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atakuwa na wajibu wa:-

i) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hizi;

ii) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

16. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo lolote la kituo kwa nia ya kukusanya ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ushuru wa mazao kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Mamlaka ya Halmashauri kutoa Mwongozo

17. Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hizi, Halmshauri itakuwa na mamlaka ya kutoa mwongozo kuhusu utaratibu wa kuendesha kituo endapo kutakuwa na haja ya kufanya hivyo.

Makosa na adhabu

18. (1) Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo mtu yeyote:-
i) atakataa au kukwepa kulipa ushuru;
ii) atashawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ushuru wa mazao;
iii) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa, Msimamizi wa kituo au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;
iv) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri, Msimamizi wa kituo au Wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa ushuru;
v) atanunua mazao katika eneo lisiloainishwa na kuidhinishwa kama kituo cha ununuzi wa mazao;
vi) atatupa au kuweka taka katika eneo lisiloruhusiwa katika kituo cha ununuzi;
vii) ataanzisha kituo cha ununuzi katika eneo ambalo halijaruhusiwa na Halmashauri; au
viii) Atanunua mazao bila kuwa na kibali cha ununuzi wa mazao
ix) Hatojisajili kama mnunuzi wa mazao katika Halmashauri; au
x) Atasafirisha mazao bila kuwa na nyaraka muhimu za mzigo kama kibali cha kusafirishia mazao nje ya Halmashauri

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Kifungu cha 18(1) atatozwa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na kisichozidi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini nan ne au adhabu zote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

19. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na kulipa ushuru anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa chini ya Kifungu cha 4(2))*

i) Ushuru wa Mazao

| Na. | Aina ya zao | Kiwango cha Ushuru (Tshs) | Ujazo kuanzia Tani Moja |
|---|---|---|---|
| 1. | Mazao ya Chakula | 3% | Bei ya kununulia |
| 2. | Mazao ya Biashara | 3% | Bei ya kununulia |

JEDWALI LA PILI

KUFIFILISHA KOSA

(Limetungwa chini ya Kifungu cha 19)

Mimi …………………………………… Nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………….. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, kwamba Tarehe ……………….. ya Mwezi ……….Mwaka …….nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha ………. cha Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo za Mwaka 2022

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha shilingi……………….badala ya kushtakiwa Mahakamani na nipo tayari kutimiza wajibu wangu kwa mujibu wa Sheria Ndogo hiyo.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe …………….. ya Mwezi …………….. Mwaka ………………………

Jina …………………………………………………

Saini ………………………………………………

Mbele ya:

Jina ………………………….. …………………………

Cheo …………………………………………………

Saini ……………………………………………………

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo iliwekwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 27-28 Aprili, 2021 na kubandikwa mbele ya:-

MOHAMED RAMADHANI
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya Nsimbo*

HALAWA MALENDEJA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya Nsimbo*

**NAKUBALI,**

L.S

Dodoma
19 Septemba, 2022

INNOCENT L. BASHUNGWA (MB.),
*Waziri wa Nchi -OR-TAMISEMI*